

## SIMANZI

# Ajali ya Shabiby, lori ilivyoua watu watano, kujeruhi

Christina Thobias,  
Mwananchi cthobias@  
mwananchi.co.tz

Iringa. Watu watano wamepoteza maisha na wengine 28 kujeruhiwa, katika ajali iliyohusisha lori lililogongana na basi la abiria la Kampuni ya Shabiby mkoani Iringa.

Kwa mujibu wa mashuhuda wa tukio hilo, lori lilionekana kupoteza mwelekeo na kuingia njia ya

basi, jambo lililosababisha magari hayo kugongana na kupinduka.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa, Dk Alfred Mwakalebela amethibitisha vifo hivyo, akisema amepokea miili ya watu watano na majeruhi 28 ambao wamepatiwa matibabu na baadhi yao kuruhusiwa.

Ajali hiyo, imetokea alfajiri ya Mei 8, 2026 katika Barabara ya Tanzania-Zam-

bia, eneo la Tanangozi, Kata ya Maseke mkoani Iringa.

## Lori lilipoteza mwelekeo

Akisimulia tukio hilo, mmoja wa mashuhuda Juma Kalinga, alisema saa chache kabla ya ajali, lori lilionekana kupoteza mwelekeo wakati likishuka kwenye mteremko mkali wa Tanangozi, kabla ya kuvamia njia ya basi.

"Nilikuwa nasikia honi ya muda mrefu tofauti na

**"Nilishtuka nikajikuta nimeangukia siti za mbele na watu walikuwa wanapiga kelele na wengine wakiwa wamebanwa."**

Mmoja wa manusura

kawaida, na ghafla nikaona lori linakuja kwa kasi huku likiyumba kutoka upande mmoja kwenda mwingine," alisema Kalinga.

Shuhuda mwingine, Yassin Mbatinga alisema baadhi ya madereva waliokuwa nyuma ya lori hilo walijaribu kusima pembeni baada ya kuona hatari iliyokuwa mbele yao na sekunde chache baadaye, ndipo mgongano ulipotokea.

"Lori lilihama njia kabisa. Ilionekana dereva anajaribu kulizua lakini breki zikawa hazishiki, ndipo likavamia upande wa basi," alisema.

Baada ya kugongana, alisema basi lilipinduka pembeni mwa barabara, na baadhi ya abiria walinasa kwenye siti na wengine wamerushwa nje.

Ameleza wananchi wa Tanangozi ndio waliokuwa wa kwanza kufika eneo la tukio kabla ya vikosi vya polisi na mamlaka nyingine na walitumia vifaa vya kawaida kuvunja sehemu za basi ili kuwaokoa majeruhi.

"Mlio ulikuwa mkubwa sana na tulipotoka nje tulikuta watu wanalia na kuomba msaada," alisema Diana Fweni, mkazi wa Mseke aliyeshiriki katika uokoaji.

Mmoja wa manusura ambaye hakutaka jina lake litajwe, alisema walikuwa usingizini kabla ya kusikia honi kali ya lori, zilizofuatiwa na kishindo kizito.

"Nilishtuka nikajikuta nimeangukia siti za mbele na watu walikuwa wanapiga kelele na wengine wakiwa wamebanwa," alisema.

Abiria mwingine, Rashid Ngezi alisema dereva wa basi alijaribu kuukwepa mgongano huo lakini hakukuwa na nafasi

ya kutosha kutokana na kasi ya lori lililokuwa likishuka.

"Lori lilikuwa linakuja kama limeachia kabisa. Dereva wa basi alijitahidi kulikwepa lakini haikuwezekana," alisema.

## Chanzo ni lori

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Iringa, Allan Bukumbi alisema uchunguzi wa awali unaonyesha dereva wa lori alishindwa kulimudu gari hilo wakati akishuka mteremko huo.

"Chanzo cha ajali hii ni dereva wa lori kushindwa kuendesha vizuri katika eneo lenye mteremko mkali. Inaonekana gari lilipoteza mwelekeo na kuvamia njia ya basi," alisema Bukumbi.

Aidha, amewataka madereva kuhakikisha magari yao yanakaguliwa kabla ya safari ili kuepusha ajali zinazotokana na hitilafu za kiufundi.

## Miili mitano

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Iringa, Dk Alfred Mwakalebela alisema hospitali imepokea majeruhi 28 pamoja na miili ya watu watano waliofariki dunia.

Alisema kati ya majeruhi hao, wanaume ni 16, wakiwamo watoto wanne, huku wanawake wakiwa 12.

Alisema baadhi wanapatiwa uangalizi maalumu kutokana na hali mbaya walizonazo.

"Mmoja wa majeruhi mwenye asili ya Asia amelazwa ICU baada ya kupata majeraha makubwa kichwani," alisema Dk Mwakalebela.

Ameongeza kuwa majeruhi 11 waliokuwa na majeraha madogo waliruhusiwa baada ya kupatiwa huduma ya kwanza.



Mwananchi akishuhudiwa basi la Shabiby likivutwa baada ya kugongana na lori katika eneo la Tanangozi kata ya Mseke mkoani Iringa. Picha na Mtandao

Wiwanda wa d...